JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

SHULE YA SEKONDARI SOYA'

S.L. P 43,

CHEMBA.

28/03/2022

Namba ya simu 0782177816.mkuu wa shule.0786642356 makamu

KUMB.Na.SSS/DO/ADM/FV/2022

MZAZI/ MLEZI WA _____

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) MWAKA WA MASOMO 2022/2023

1.0 UTANGULIZI

Walimu, wafanyakazi na wanajumuiya ya shule ya sekondari Soya wanayofuraha kukujulisha kuwa kijana wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO mwaka wa masomo 2022/2023 katika shule ya sekondari Soya na. atasoma mchepuo wa PCM / PCB. Muhula wa kwanza utaanza tarehe 5/9/2022 na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 12/9/2022.

NB.Mzazi azingatie kama kutakuwa na mabadiliko ya tarehe ya kufungua shule yatakayotolewa na serikali.

2.0 MAHALI SHULE ILIPO NA JINSI YA KUFIKA

Shule ipo kijiji cha Magandi kilichopo kata ya Soya, Tarafa ya Goima, wilaya ya Chemba na mkoa wa Dodoma. Uwapo Dodoma unaweza kupanda basi la kutoka Dodoma-Soya katika standi ya mabasi ya Chang'ombe kila siku saa 6:00 mchana (isipokuwa Jumapili). Aidha, pia unaweza kufika Soya sekondari kwa kupanda basi la Soya katika stendi ya mabasi Kondoa mjini. Nauli ya

kutoka Dodoma mjini hadi Soya ni Tsh.10,000/=.na kondoa –Soya ni Tsh. 5000/=. Unaweza piakushuka chemba mjini (wilayani) na kupanda mabasi yanayotoka kondoa nauli ni Tsh.5000/=

3.0 ADA NA MICHANGO MBALIMBALI.

Kila mwanafunzai anapaswa kulipiwa ADA/ MICHANGO IFUATAYO;

(i) Tahadhari Tsh. 5000/= inalipwa mara moja tu

(ii) Mpishi na kuni Tsh. 20,000/= kwa mwaka.

(iii) Huduma ya maji Tsh. 15,000/= kwa mwaka.

(iv) Huduma ya umeme Tsh. 10000/= kwa mwaka.

(v) Kuboresha taaluma Tsh. 20,000/= kwa mwaka.

(vi) Mchango wa mlinzi Tsh. 10,000/= kwa mwaka.

(vii) Mchango wa ukarabati wa samani Tsh 10,000/=. Kwa mwaka.

(viii) Mchango wa mahafali Tsh. 10,000. Inalipwa mara moja tu.

(ix) Mchango wa kununua kemikali Tsh. 10000/= kwa mwaka.

(x) Mchango wa UMISETA Tsh. 5000/= kwa mwaka.

(xi) Ada Tsh. 70000/= kwa mwaka au Tsh. 35000/= kwa muhula.

NB: 1.Fedha za ada na michango yote weka kwenye akaunti ya Soya Sekondari **A/C NA. 50201200082** benki ya **NMB** na utuletee Pay in slip.

Jumla ya fedha anazotakiwa mwanafunzi kulipiwa kabla ya kuanza masomo isipungue Tsh. 150,000/= kwa mhula au zote 185,000/= (ada na michango)

4. **SARE YA SHULE.**

(i) Suruali mbili (02) za rangi nyeusi (zenye rinda mbili kila upande, upana wa chini saizi 16. (zingatia upana huu utakaguliwa siku ya kuripoti).

(ii) Mashati mawili (02) meupe yenye mikono miarefu

(iii) Soksi rangi nyeusi jozi mbili (02)

(iv) Viatu vyeusi vya kufunika vyenye Kamba jozi mbili (02)

(v) Tai ndefu rangi nyeusi (mbili)

(vi) Sweta rangi ya kijivu (kuna baridi kuanzia mwezi wa sita.

(vii) Track suit ya blue bahari

(viii) Sare ya kushindia (shamba dressing) suruali ya khaki na T- shirt ya rangi ya blue yenye nembo ya shule. (Tshirt zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 15000/= kwa T- shirt moja)

NB: Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa na mavazi mengine yoyote Zaidi ya yaliyoelekezwa na anatakiwa kuwa katika mavazi hayo muda wote awapo shuleni au katika mazingira ya nje ya shule kwa ruhusa. Hii izingatiwe sana.

5.0 MAHITAJI MENGINE

Kila mwanafunzi anakiwa kuja na mahitaji yafuatayo;

(i) Bunda (ream) mbili za karatasi za A4

(ii) Shuka mbili (02) za rangi ya pinki au buu bahari

(iii) Mto na foronya yake (rangi ya foronya ifanane na rangi ya shuka)

(iv) Ndoo mbili (02) za ujazo wa lita kumi kwaajili ya kutunzia maji ya kunywa na kuogea

(v) Kijiko, bakuli, sahani na kikombe

(vi) Madaftari makubwa kuanzia nane na kalamu za kuandikia .

(vii) Scientific calculator

(viii) Kitambulisho cha bima ya afya

(ix) Laboaratory coat nyeupe kwaajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya vitendo.

(x) Godoro la $2\frac{1}{2}$ ft na chandarua

(xi) Sanduku la kutunzia vifaa vyake

(xii) Dissecting kit moja kwa mchepuo wa PCB ni muhimu

(xiii) Vitabu vya mchepuo anaosoma. Tunasisiza kuwa na vitabu vilivyotolewa na Taasisi ya Elimu Tanzaania.(TIE) na vingine kama CHANDI.

(xiv) Vifaa vya michezo: bukta na fulana rangi ya bluu au nyekundu zenye ufito mweupe

(xv) Fedha ya kitambulisho sh.6000 italipwa keshi.

Baadhi ya vifaa unaweza kuvipata katika duka la shule, vifaa hivyo ni pamoja na ndoo, vijiko , bakuli, sahani, vikombe, madaftari, na dissecting kit kwa Tsh 25000/=.na Aidha unaweza kununua godoro kweye maduka yaliyo jirani na shule kwa bei ya Tsh.40,000

6.0 VIFAA VYA USAFI.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwaajili ya kufanyia usafi.

(i). fagio la ndani lenye mpini mrefu(soft bloom) moja (01)

(ii) Fagio gumu la chooni lenye mpini (hard bloom) moja (01)

(iii) Fagio la chelewa lenye mpini mrefu moja (01)

(iv) Fagio refu la kutolea buibui moja (01).

(v) Squeezer (mpira wa kukaushia maji) -01

(vi) Brush ya kusugulia choo yenye mpini mfupi

(vii) Jembe na mpini wake -01

(viii) Ndoo kubwa -01

(ix) Slashe -01

(x) Panga -01

NB: Vifaa vyote vya usafi vitapokelewa siku ya kuripoti au unaweza kuwasilisha fedha taslimu Tsh. 50,000/=

7.0 SHERIA ZA SHULE.

Mara ufikapo shuleni, utapewa nakala ya sheria za shule, ambazo zinasisitiza utii, heshima, na maadili na uzalendo. Zifuatazo na sheria za msingi za shule;

(i) NI LAZIMA kuhudhuria darasani vipindi vyote.

(ii) Kuheshimu walimu, wafanyakazi na viongozi mbalimbali.

(iii) Ni lazima kuvaa sare ya shule wakati wote ukiwa katika eneo la shule na nje ya eneo la shule.

(iv) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza mali za shule.

(v) Kuzingatia usafi wa madarasa, mwili, mavazi, nywele, mabweni, viwanja vya michezo, na maeneo yote ya shule.

(vi) Ni marufuku kufuga nywele ndefu, ndevu, kucha, na kuvaa mapambo.

(vii) Mwanafunzi haruhusiwi KUMILIKI/ KUWA NA SIMU, redio, heater, pasi ya umeme na siraha yoyote, atakayebainika adhabu kali itachukuliwa dhidi yake.
(viii) Ni marufuku kupiga kelele madarasani na mabwenini.

(ix) Mwanafunzi haruhusiwi kupika bwenini.

(x) Ni marufuku kumpeleka mgeni bwenini.

(xi) Kila mwanafunzi aishi katika bweni na chumba alichopangiwa.
(xii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa ,na nyimbo za uzalendo.

8.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi

(ii) Ulevi wa aina yoyote

(iii) Uvutaji wa bangi / madawa ya kulevya

(iv) Uasherati

(v) Makosa ya jinai

(vi) Kupigana au kupiga

(vii) Kuoa

(viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma

(ix) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa

(x) Kusababisha mimba

(xi) Utovu sugu wa nidhamu

(xii) Utoro wa shule wa muda mrefu

(xiii) Kuandaa, kuchochea au kusababisha mgomo shuleni

(xiv) Kuchochea na kusababisha vurugu za ubaguzi wa dini, jinsia, ukabila.nk

(xv) Kutoroka na kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule
(xvi) Kugomea adhabu
(xvii) Kuunganisha umeme kinyume na taratibu za shule.
(xviii) Kufanya vikao visivyo halali / rasmi bila kibali cha mkuu wa shule.

KARIBU SANA SOYA SEKONDARI

……
MOKIWA PETRO
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SOYA

HATI YA MAKUBALIANO

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI SOYA,

KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHART YA SHULE

Mimi……

nakubali nafasi ya kidato cha..... niliyopewa katika shule yako.

Ninayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizopo na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi nitawaheshimu na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi wengine kama walezi wangu.

Naahidi kuwa nitawatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.

Ninaahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu na nitajielimisha kwa nguvu zangu zote na akili yangu yote kwa manufaa yangu binafsi na kwa manufaa ya Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shuleni.
JINA LA MWANAFUNZI…...SAINI ……
JINA LA MZAZI/MLEZI……SAINI……

Anwani ya mzazi/mlezi……

Namba ya simu ……Email……

Namba ya kuandikishwa……Tarehe…….

Darasa alilopangiwa……..……

Jina la mwalimu wa darasa……..Saini……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
CHEMBA DISTRICT COUNCILI
SOYA SECONDARY SCHOOL.

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(TO be filled by medical officer in respect of all form V entrants)

Student's full name……

Age ……years. Sex……

Blood count (red and white)……

Stool examination……

Syphilis and other venereal diseases
test……..

T.B test……

Eye test……

Ear test……

Spleen …….....

Abdomen …….....

Urine ……..

ADDITIONAL INFORMATION

(If any) e.g. physical defects important,

Infections, chronic or family diseases etc.……

I certify that the above student is fit to pursue studies at Soya secondary school

Station……..Signature…….

Date…….Designation……Official stamp……

NB: This form should be completed and submitted to school on arrival.